JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA

SHULE YA SEKONDARI YA WAVULANA CHEMBA

S.L. P 830 CHEMBA

SIMU NA. 0763292559/0782177816 MKUU WA SHULE

0756961623 M/MKUU WA SHULE

0711967018/0620612696 M/ TAALUMA .

Mzazi/ Mlezi………………………………………………………………………………………

Anuani: S.L.P ……………………………………………………………………………c/o…………

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI YA WAVULANA CHEMBA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA MWAKA 2026.**

1. Kwa niaba ya jumuiya nzima ya shule ya sekondari ya wavulana Chemba,nampongeza mwanao kwa kuchaguliwa kujiunga na shule yetu. Hongera sana na karibu sana.
2. MAELEKEZO YA KUFIKA SHULENI:
   Shule ya sekondari ya wavulana Chemba ipo katika kata ya Chemba, tarafa ya Goima ,wilaya ya Chemba. Kufika shuleni ukitokea Dodoma mjini panda mabasi yanayoenda Kondoa na shuka kituo cha Chemba mjini, shule ipo karibu na chuo cha ufundi cha VETA Chemba. Nauli ya kutoka Dodoma mjini hadi Chemba ni Sh.7000/= Mabasi yanayoenda Kondoa yanapatikana njia panda ya "Area C" standi ya machame na Machimulas.
   Kwa anayetoka barabara ya Arusha shuka kituo cha Chemba mjini ukitokea Kondoa.
3. SIKU YA KUFUNGUA SHULE:
   Shule itafunguliwa tarehe……………. mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe…………………Mwanafunzi anapokuja shuleni aje na barua hii kwaajili ya utambulisho. (**Mwanafunzi afiken siku moja kabla ya kuanza masomo kwa tarehe itakayotangazwa na serikali)**
4. MAHITAJI MUHIMU YA SHULE:
   A:SARE ZA SHULE
   (i) Mashati mawili (2) meupe yenye mikono mifupi na mfuko mmoja upande wa kushoto.
   (ii) Suruali mbili (2) rangi ya khaki yenye upana unaoridhisha.
   (iii) Vazi la nje ya darasa T- shirt isiyo na kola rangi ya kijivu yenye nembo ya shule na suruali rangi ya kijani-( unaweza kupata T shirt na suruali kwenye maduka yaliyo karibu na shule

(iv) Sweta rangi ya kijani jeshi-( unaweza kupata kwenye maduka yaliyo karibu na shule)
(v) Tai ndefu rangi ya khaki ziwe (mbili)
(vi) Soksi za rangi nyeusi jozi mbili au zaidi
(vii) Viatu vya shule vya ngozi rangi nyeusi vya kufunga na kamba jozi mbili, kiwi, na brashi.

B: **VIFAA VINGINE**

Madaftari makubwa (counter book) kumi (10)

i. Kalamu ya wino wa bluu au mweusi 10 au zaidi, penseli kifutio na rula
ii. Mkebe kwa masomo ya sayansi.
iii. Kamusi ya kiingereza (oxford dictionary).
iv. Bunda mbili za karatasi (ream).
v. Ndoo mbili (2) za lita 10 kwaajili ya kutunzia maji na kufanyia usafi na lita moja ya sabuni ya maji.
vi. Fagio moja la ndani (soft broom), chelewa moja hard broom na moper/skuizer moja
vii. Jembe moja lenye mpini mrefu na fyekeo moja
viii. Godoro lenye upana wa futi 2.5 x6
ix. Shuka mbili za rangi ya bluu bahari
x. Chandarua nyeupe ukubwa wa 3.5

C: **MAVAZI YA MICHEZO**

i. Tracksuit moja rangi nyeusi.
ii. Raba nyeupe jozi moja.
iii. Bukta na T-shirt rangi ya bluu yenye ufito mweupe.

D: **MAHITAJI MENGINE.**

i. Vyombo vya chakula; Sahani, bakuli,kikombe,(aina ya mfupa) na kijiko
ii. Nguo za ndani za kutosha, dawa ya meno, sabuni ya kufulia mafuta ya ngozi ya kupaka.
**iii.** Kadi ya bima ya afya ya NHIF. **(Hii ni muhimu sana kwani gharama za matibabu wakati mwingine huwa juu)**
iv. Sanduku imara (trunker)
v. Picha mbili ukubwa (pass poti saizi)

5. KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu Nchini. Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo ambayo kwa pamoja yanaunda sheria za Shule;

i. Kuheshimu viongozi, walimu na wazazi pamoja na wanafunzi wenzako na jumuiya nzima ya shule wakiwemo walinzi na wapishi .
ii. Kuhudhuria vipindi vyote vya darasani pamoja na kazi za nje ya darasa.
iii. Kushiriki kikamilifu vipindi vyote vya usiku ( preparation )
iv. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani ya eneo la shule wakati wote isipokuwa kwa ruhusa maalumu.
v. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
vi. Kuwahi shuleni baada ya likizo yaani kuripoti kwa wakati kwa tarehe iliyopangwa na si vinginevyo
vii. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
viii. Kuvaa sare ya shule wakati wote ukiwa ndani ya eneo la shule au nje ya shule kwa ruhusa.
ix. Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki vitu vyenye ncha kali hususan kisu.
x. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

1. **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi** .
2. **Mwanafunzi awapo shuleni atapaswa kulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa**. Ni marufuku wanafunzi wawili kulala kitanda kimoja au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika kwa mwanafunzi mmoja tu.
3. **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa Mkuu wa shule tu**.

3.2.Makosa yatakayosababisha mwanafunzi kufukuzwa shule ni pamoja na:

i. Wizi

ii. Kutokuhudhuria masomo kwa zaidi ya siku tisini (90) bila taarifa/ Utoro

iii.Kugoma na kuhamasisha mgomo.

iv.Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.

v.Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.

vi.Kufuga ndevu

vii.Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya.

viii.Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya.

ix. Kusababisha mimba na kushiriki vitendo vya ushoga.

x.Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa, na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.

xi.Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.

xii.Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.

xiii. Kudharau Bendera ya Taifa na Wimbo wa Taifa

xiv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kwa kunywa sumu.

xv. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi

**Viambatisho na fomu muhimu**

i. Fomu ya uchungunzi wa afya ( medical examination form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya Serikali.
ii. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa mwanafunzi wa kutoshiriki katika mgomo, fujo, na makosa ya jinai
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WAVULANA CHEMBA (CHEMBA BOYS' SECONDARY SCHOOL)

Saini ya mkuu wa shule…………………………………

Jina la mkuu wa shule: MOKIWA .P. JOSEPH

NB:**Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli ( wizi kwa njia ya mtandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakipigiwa simu au kutumiwa ujumbe mfupi wa simu (sms) na watu wanaojitambulisha kama ni walimu walio chini ya mkuu wa shule. Watu hawa huwaambia wazazi kuwa mtoto wao ni mgonjwa au ana shida kubwa. Naomba wazazi na walezi wapuuzi e ujumbe huu.**

**Fomu.Na. 1 AHADI YA MZAZI/MLEZI**

Mimi……………………………………………………………………………..wa S.L.P ………Simu ……..ya mkononi namba……………………………………na mwenye picha hapo juu. Kazi yangu ni……………………………………………..

Natamka hapa kama mzazi/ mlezi wa……………………………………………………….Ninakubali kwa hiari yangu mwanangu asome katika shule ya sekondari ya wavulana Chemba kuanzia tarehe…………………………………

Ninaahidi kama ifuatavyo:

1. Kwamba nimekubali chaguo alilopewa mwanangu .
2. Ninaahidi kumpatia mwanangu vifaa vyote kama ilivyoainishwa katika fomu ya kujiunga.
3. Ninatambua kuwa walimu wanahitaji ushirikiano wangu katika kumpatia mwanangu elimu na nitashirikiana nao bega kwa bega kwa masuala yanayohusu mwanangu kitaaluma na nidhamu ili aweze kufikia malengo yake na ya Taifa.
4. Ninaahidi kuwa endapo mwanangu ataenda kinyume na taratibu zilizoainishwa katika fomu hii achukuliwe hatua stahiki za kinidhamu kama ilivyooneshwa.
   Jina:…………………………………………………Sani…………………………………………………………………..
   Tarehe:……………………………………………Uhusiano na mwanafunzi……………………………..

   Fomu Na. 2. AHADI YA MWANAFUNZI

   Mimi mwanafunzi……………………………………………………………………………..wa kidato cha kwanza mwaka 2026. Ninakiri kusoma, kuelewa na kuahidi kutii taratibu zote zilizoainishwa katika fomu iliyotumwa kwangu na mkuu wa shule ya sekondari Chemba Boys’. Nitatoa ushirikiano kwa walimu wangu na shule kwa ujumla katika muda wangu wote nitakaokuwa shuleni.

Jina: ………………………………...                Saini ______________________

Tarehe: ____________________

Fomu.Na. 3

KIAPO CHA MZAZI/MZAZI.

Mimi: ______________________________ wa S.L.P ____________ ________ Mji

Na. ____________________ .Nakiri kukaa na kuzungumza na mwanangu juu ya taratibu na sheria za shule na ninaahidi kumsaidia na kutoa ushirikiano wa kutosha kwa mkuu wa shule na walimu kwa muda wote ambao mwanangu atakapokuwa katika shule hii. Ninatambua madhara ya mwanangu kutembelewa na wageni wasioeleweka wakati akiwa shuleni na ninaomba shule iwatambue watu watatu (3) ambao wanahusika katika muda wote ambao atakuwa shuleni nao ni :-( ambatanisha picha passport size zao).

1. Jina:………………………………………………………………
   Kazi…………………………… Makazi……………………….
   Uhusiano na mwanafunzi……………………………….Namba ya simu……………………………………………………

2. Jina:…………………………………………………………………
   Kazi……………………………..Makazi……………………….
   Uhusiano na mwanafunzi…………………………………  Namba ya simu………………………………………………

3. Jina:………………………………………………………………
   Kazi…………………………… Makazi……………………….
   Uhusiano na mwanafunzi……………………………….Namba ya simu……………………………………………………

**PRIME MINISTERS' OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**CHEMBA DISTRICT COUNCIL**

## CHEMBA BOYS' SECONDARY SCHOOL.

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

(To be filled by medical officer in respect of all form one (I) entrants)

Student's full name……………………………………………………………………………

Age …………………………………years. Sex………………………………………………

Blood count (red and white)……………………………………………………………………

Stool examination………………………………………………………………………………

Syphilis and other venereal diseases test…………………………………………………….

T.B test……………………………………………………………………………………………

Eye test……………………………………………………………………………………………

Ear test……………………………………………………………………………………………

Spleen …………………………………………………………………..................................

Abdomen ……………………………………………………….............................................

Urine for plamotest………………………………………………………………………………

**ADDITIONAL INFORMATION**

(If any) e.g. physical defects (impairment)Infections, chronic or family diseases etc.

I certify that the above student is fit to pursue studies at Chemba Boys secondary school

Station…………………..Signature………………….

Date…………………….Designation……………………Official stamp…………………………

NB: This form should be completed and submitted to school on arrival.